# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo humo, kwakutujaalia uhai na afya njema, ambapo leo hii tumewezesha kukutana tena katika Baraza hili Tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, napenda kukushukuru Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awazidishie busara na hekima katika kutekeleza jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Uongozi mzima wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawasisitiza wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ufanisi zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudia.

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa namna ya kipekee pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Nassor Salim Ali | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| *8.* | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kanuni ya 109(18) ya Kanuni za kudumu za Baraza la wawakilishi Toleo la 2020, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Utekelezaji wa Ushauri na Mapendekezo kwa Wizara ya Habari,Vijana,Utamaduni na Michezo ambapo jumla ya mapendekezo 41 yaliyowasilishwa kwa Wizara yote tunashukuru yameweza kupatiwa majibu.

## SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZANZIBAR (ZBC)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara na Shirika la Utangazaji ZBC, kwa kukamilisha taratibu za uwandaaji wa muundo mpya wa Shirika na kuuwasilisha Tume ya Utumishi Serikalini kwa hatua za kiutendaji ambapo Muundo huo umezingatia kasoro zote zilizo bainika

katika muundo wa zamani.

**Mheshimiwa Spika,**

Mbali na mafanikio ya Shirika la Utangazaji ZBC, bado kuna changamoto kubwa ya jengo la ofisi kwa upande wa ZBC Dar es Salaam hali inayopelekea usumbufu kwa wafanyakazi. Hivyo, Kamati inapendekeza tena kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo kuwatafutia jengo la kudumu kituo cha ZBC Dar Es Salaam licha ya kuwa wameongezewa nafasi nyengine katika jengo hilo wanalotumia kwa sasa.

Kufuatia kuwepo kwa changamoto ya Sheria ya Shirika la Utangazaji Nam. 4 ya Mwaka 2013 zinazopelekea ucheleweshaji katika utekelezaji wa majukumu ya Shirika hilo, Kamati inaishauri Wizara kuifanyia mapitio na kukamilisha marekebisho ya sheria ili iweze kurahisisha kazi zifanyike kwa wepesi na ufanisi kama inavyotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeelezea wasi wasi wake kuhusu hatua zilizofikiwa katika utaarishaji wa Kanuni ya Sheria nambari 4 ya Shirika la Utangazaji ZBC ya Mwaka 2013, baada ya kukamilika kwa taratibu zote kwa mujibu wa sheria. Kamati inashauri Wizara kukamilisha uwasilishwaji wa Kanuni hizo kwa Mwanasheria Mkuu kama taratibu zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipendekeza uajiri wa watendaji wapya wa Shirika akiwemo Dereva katika Kituo cha ZBC, Dar Es Salam ili kuondoa changamoto ya ufinyu wa madereva. Kamati inashauri Tume ya Utumishi Serikalini kuharakisha kutoa vibali vya uajiri ili kukidhi mahitaji ya watendaji katika Kituo hicho cha Shirika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza hatua ya Wizara kwa kufanikiwa kupata eneo la ujenzi kwa ajili ya Jengo la kudumu la Ofisi ya Tume ya Utangazaji Zanzibar.

Sambamba na hilo, Kamati inaipongeza Kampuni ya usambazaji wa Maudhui ya (ZMUX)

kwa kuandaa Mpango wa uwekezaji wa Taasisi hiyo. Mpango huo utaiwezesha Kampuni kutotegemea ruzuku kutoka Serikalini na kuweza kutoa gawiwo kwa Serikali.

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na Kamati kuridhishwa na utekelezaji wa Wizara kupitia Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kuanza kusambaza Magazeti katika Bandari kuu ya Zanzibar, Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Magazeti Zanzibar kusimamia maamuzi yaliotolewa na Serikali kuhusu ulipwaji wa deni kubwa la usambazwaji wa magazeti kwa taasisi zote za SMZ na SMT.

Kamati inasisitiza tena kwa Wizara kuziandikia tena barua taasisi zote za Serikali na Binafsi kuwakumbushia tena walipe deni hilo ili Shirika liweze kujiendesha wenyewe na kuacha kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Shirika kwa muda mrefu limekuwa likidai zaidi ya shilingi Bilioni 2 kwa Taasisi za Serikali ikiwa ni malipo ya magazeti yake. Pia Kamati inaishauri Serikali kuwa na wigo mpana katika kutafuta masoko ya mauzo ya magazeti yake kwa kutumia njia za mitandao ya kijamii ili kwenda sambasamba na wakati uliyopo.

## WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI ZANZIBAR (ZGP)

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaiomba Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kushirikiana na Wizara ya Habari ili kuweza kukamilisha suala la uajiri wa nafasi sita ambazo watumishi wake wamestaafu ili kuzijaza nafasi hizo na waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa kipaumbele suala la ununuzi wa mitambo mipya na ya kisasa kwa Wakala wa Serikali

wa Uchapaji kwani fedha hizo zimeidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Kamati haijaridhishwa na ucheleweshwaji wa kupatiwa fedha hizo Wakala, Hivyo Kamati inaishauri Wizara husika katika mwaka wa fedha 2023/24 kuwaingizia Wakala wa Uchapaji wa Serikali Bajeti ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri Serikali kumpatia Wakala wa Uchapaji Ghala la kudumu kuhifadhia mali ghafi na bidhaa zinazonunuliwa au kuzalishwa na Wakala, Ghala linalotumika hivi sasa ni la kuanzimwa kwa muda.

## BARAZA LA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kulipa kipaumbele Baraza la Michezo kwa kuwapatia fedha ili kuweza kuinua vipaji vya michezo kwa vijana wetu waweze kupata ajira kupitia michezo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati.

Kwa niaba ya Kamati yangu pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikiwasilisha Hotuba hii. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili na waichangie hotuba hii kwa mustakabali wa nchi yetu na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.

……………………….

**Mhe. Sabiha Filfil Thani**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**Zanzibar.**